-JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE

SHULE YA SEKONDARI MULUNGA,
S.L.P 865,
NJOMBE
27/11/2020

Kumb.Na.MUSS/E.09/F1/03
……..
…….
Ndugu,

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI MULUNGA MWAKA 2020**

1. UTANGULIZI

Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Mulunga mwaka 2021. Shule ipo katika tarafa ya Lupembe, Kata ya Ukalawa, Kijiji cha Ukalawa umbali wa kilometa 103 kutoka njombe mjini. Usafiri wa basi kutoka mjini Njombe unapatikana katika kituo cha mabasi cha Njombe nauli ni Tsh. 9,000/=. Wanafunzi wote waliochaguliwa kidato cha kwanza watatakiwa kuripoti shuleni tarehe 11/01/2021 bila kukosa wakiwa na wazazi /walezi wao pamoja na mahitaji yote, usajili utafanyika siku hiyo.

2. SARE ZA SHULE

a) WASICHANA

i. Sketi mbili ndefu mshono linda boksi mbele na nyuma. Moja iwe rangi ya damu ya mzee na nyingine dark blue. Sketi zote ziwe za kitambaa cha isitimu namba moja. Vitambaa vimeambatanishwa.
ii. Mashati mawili meupe ya mikono mirefu.
iii. Sweta moja rangi ya kijivu.
iv. Viatu vyeusi jozi mbili vya ngozi vya kufunga na kamba (sio yeboyebo au bajaji) vyenye visigino vya kawaida.
v. Soksi jozi nne rangi nyeupe.
vi. Lesso mbili (02).
vii. Nguo za ndani zisipungue sita (06).

b) WAVULANA

i. Mashati mawili meupe ya mikono mirefu.
ii. Suruali mbili. Moja rangi ya damu ya mzee na nyingine ya dark blue. Mshono wa kawaida mifuko mitatu na iwe na tanapu. Vitambaa vimeambatanishwa.
iii. Sweta moja rangi ya kijivu.
iv. Mkanda wa suruali wa ngozi.
v. Viatu vyeusi jozi mbili vya ngozi vya kufunga na kamba (sio yeboyebo au bajaji) vyenye visigino vya kawaida.
vi. Soksi jozi nne rangi nyeusi.
vii. Lesso mbili (02).
viii. Nguo za ndani zisipungue sita (06).

c) VAZI LA WANAFUNZI WAISLAMU
   i. Kitambaa cha kichwani “Hijab” cheupe kisicho na marembo kwa wasichana.
   ii. Nusu kanzu nyeupe kitambaa cha tetroni kwa wavulana.

d) NGUO ZAMICHEZO
   i. Raba jozi moja
   ii. Bukta moja (wavulana)
   iii. T- shirt ya blue moja
   iv. Track suit nyeusi moja yenye mistari mieupe.

3. VIFAA VYA MASOMO

a. “Counter books 3 - quire au 4 - quire” ziwe kumi na moja (11).
b. Mathematical set/mkebe mmoja wenye vifaa vyote ndani.
c. Kalamu za kutosha (angalau 10 za wino bluu au nyeusi na 3 za mkaa)
d. Mfuko(begi) la kubebea daftari. Mifuko ya plastic hairuhusiwi.
e. Rula ndefu moja isiyo ya rangi yenye sentimeta 30.

4. MAHITAJI YA WANAFUNZI WA HOSTEL(WASICHANA TU)

a. Godoro Dodoma au Tan fomu moja la futi $2\frac{1}{2}$ lenye foronya na mto wake. Aina nyingine ya godoro hairuhusiwi na haitapokelewa.
b. Blanketi moja (1) nzito.
c. Shuka mbili moja rangi ya pinki na nyingine rangi ya bluu.
d. Mswaki na dawa ya meno, sabuni za kutosha miche isiyopungua mitatu, kiwi na brashi, kitana, taulo, kandambili, mafuta ya kupaka na torchi ndogo. Perfume, lotion, angle face n.k haviruhusiwi.
e. Ndoo kubwa lita 20 moja ya kutunzia maji, na kindoo kidogo cha lita 10 kimoja cha kuogea. Ndoo zote ziwe za bluu, rangi nyingine haikubaliki kwani kila kidato kina rangi yake ili kupunguza wizi wa ndoo.
f. Gauni mbili ndefu. Moja rangi ya damu ya mzee lenye baby colar dark blue, lingine rangi ya dark blue lenye baby colar damu ya mzee, yote kitambaa cha isitimu namba 1 na mshono linda box mbele na nyuma.
g. Chandarua kimoja cha upana futi $2\frac{1}{2}$.

5. MAAGIZO MUHIMU KWA WOTE

a. Aje na jembe jipya lenye mpini mpya kwa ajili ya usafi
b. Awe na bima ya afya CHIF au NHIF.
c. Awe na fedha kidogo ya mahitaji.
d. Wanafunzi wote wa kike ni lazima kuishi hosteli.
e. Aje na kikombe cha nusu lita chenye mshikio, sahani, bakuli na kijiko kwa ajili ya chakula. Container, hotpot n.k haviruhusiwi.

6. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa mara baada ya kuripoti shuleni:-

a. MAMBO YA KUZINGATIA
   i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wenzako na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
   ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.

iii. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation) au muda wa ziada mwingine wa kujisomea utakaowekwa.
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi, na mazingira ya shule.
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
ix. Kulinda na kutunza mali za umma.

b. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE:-
i. Wizi
ii. Uasherati, ubakaji na ushoga
iii. Ulevi na matumizi mabaya ya madawa ya kulevya
iv. Uvutaji wa bangi
v. Makosa ya jinai
vi. Kupigana au kupiga
vii. Kuharibu makusudi mali ya umma
viii. Kudharau Bendera ya Taifa
ix. Kuoa au kuolewa
x. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
xi. Kutoa mimba
xii. Kugoma, kuchochea na kuongoza kuvuruga amani na usalama wa watu
xiii. Kukataa adhabu kwa makusudi
xiv. Lugha za matusi
xv. Utoro wa muda mrefu
xvi. Kuto kufanya mazoezi au mitihani na kutega vipindi
xvii. Kiburi na ukaidi
xviii. Kulawiti.

MUHIMU:- Kumbuka kuja na nakala ya cheti cha kuzaliwa, fomu ya kupimwa afya, Fomu ya utunzaji vifaa, samani, miundombinu na mali za shule na fomu ya kukubali kujiunga na sekondari.

Hongera kwa kupata nafasi hii adimu na karibu sana Mulunga sekondari.

……..
MEKLAUD ISACK KYANDO
MKUU WA SHULE

FOMU YA KUJIANDIKISHA SHULENI

A. KUKUBALI KUJIUNGA NA MASOMO YA SEKONDARI

Mimi …….(majina matatu) wa kijiji cha …….
Nimefaulu na kuchaguliwa kujiunga na masomo ya sekondari kwenda shule ya sekondari ya ……..
Kutoka shule ya msingi ya …….. Nakubali kujiunga na masomo ya sekondari mwaka …… na kuwa nitafuata na kutii sheria, kanuni na taratibu zote za shule.
Ahsante.

Sahihi …… Tarehe …./…./…….

B. HABARI ZA MWANAFUNZI

a. Jina la mwanafunzi: ……
b. Mahali ulipozaliwa wilaya: …… Mkoa ……..
c. Tarehe ya kuzaliwa …….
d. Dini …… Dhehebu ……..
e. Shule uliyotoka …….
f. Shughuli unazopendelea mbali na masomo kama vile mpira wa miguu, mpira wa mikono, riadha, kuimba n.k …….

Sahihi ya mwanafunzi …….. Tarehe ……..

C. HABARI ZA WAZAZI

i. Baba yu hai …. ……Ndiyo/hapana simu …….
ii. Mama yu hai ……ndiyo/hapana simu …….
iii. Jina la mzazi/mlezi anayekulea ……. simu ……..
iv. Uhusiano wako na mlezi ……..
v. Kazi ya mzazi/mlezi ……
vi. Anwani ya mzazi /mlezi ……. Simu ……
vii. Mahali ambapo mzazi/mlezi anaishi
Kijiji/mji ……..... Kata …….
Tarafa …… Wilaya …….. Mkoa …….
Sahihi ya mzazi/mlezi …….. Tarehe ……..

D. NDUGU WENGINE WA KARIBU

JINA	UHUSIANO	ANWANI YAKE	SIMU
1……	……	…….	……..
2……	……	…….	……..
3……	……	…….	……..

E. OFISI YA MTENDAJI KATA AU MWENYEKITI WA MTAA/KIJIJI AMBAKO MZAZI AU MLEZI WA MWANAFUNZI ANAISHI

i. Jina …… Kata ya ……
Anuani ……. Simu ……

ii. JIna …….. Kijiji cha ……..
Anuani …….. Simu ……..

PRESIDENT'S OFICE – REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
NJOMBE DISTRICT COUNCIL

MULUNGA SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 865,
NJOMBE

REF.NO. MUSS/E.09/F1/02
THE MEDICAL OFFICER,
……..,
……..,
…….

RE**: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

Please kindly examine (Name) ……...
to determine her/his physical and mental fitness for pursuing secondary school studies.

1. Eyesight ……
2. Hearing ……
3. Speech ……
4. Limbus ……
5. Leprosy ……
6. Epilepsy ……
7. Cardiac diseases ……..
8. Rheumatism ……..
9. Venereal diseases ……..
10. Pregnancy (for girls) …….
11. Any other serious diseases …….

I certify that the above named is fit/unfit to pursue his/her studies as required:-
Designation ……
Station ……
Signature ……
Date ……
Stamp ……

FOMU YA UTUNZAJI SAMANI, VIFAA, MIUNDOMBINU NA MALI ZA SHULE

A. KUKUBALI KUTUNZA SAMANI, VIFAA, MIUNDOMBINU NA MALI ZA SHULE

i) MWANAFUNZI

Mimi …….(majina matatu) wa kijiji cha …….

Ninaahidi kuwa nitatunza samani, vifaa, miundombinu na mali za shule ya sekondari Mulunga kwa muda wote nitakaokuwa mwanafunzi wa shule hii. Ninafahamu kuwa kuharibu miundombinu ya shule/kuvunja ama kupoteza samani, vifaa na mali za shule ni kosa kisheria nitakuwa tayari kuajibishwa kwa makosa hao.

Ahsante.

Sahihi …… Tarehe …./…./…….

ii) MZAZI/MLEZI

Mimi …….(majina matatu) ambaye ni mzazi/mlezi wa mtoto tajwa hapo juu wa kijiji cha ……..

Ninaahidi kuwa nitawajibika endapo patatokea uharibifu wa miundombinu, samani, vifaa, mali ama upotevu.

Ninafahamu kuwa kuharibu miundombinu ya shule/kuvunja ama kupoteza samani, vifaa na mali za shule ni kosa kisheria na mimi kama mzazi/mlezi nitakuwa tayari kuajibishwa kwa makosa yatakayokuwa yamefanywa na mtoto wangu.

Ahsante.

Sahihi …… Tarehe …./…./…….

B. OFISI YA MTENDAJI KATA AU MWENYEKITI WA MTAA/KIJIJI AMBAKO MZAZI AU MLEZI WA MWANAFUNZI ANAISHI

i. Jina …… ……. Kata ya ……

Anuani ……. Simu ……

ii. JIna …….. …… Kijiji cha …….

Anuani …….. Simu …….

Tarehe …./…../……